POSITIVE THINKERS TANZANIA

4th Floor, Mavuno House, P.O. BOX 78668,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 766 606162
Barua pepe: info@positivethinkers.or.tz
Tovuti: www.positivethinkers.or.tz

RIPOTI YA UTAFITI:

VIGEZO NA MATARAJIO YA WANANCHI KATIKA KUFANYA MAAMUZI YA KUCHAGUA VIONGOZI KUELEKEA UCHAGUZI MKUU 2015, TANZANIA.

March 2015

Vielelezo Katika Jedwali ii
SHUKRANI iii
MUHTASARI WA UTAFITI iv
1.0. UTANGULIZI 1
2.0. MAELEZO YA POSITIVE THINKERS TANZANIA 2
3.0. MELEZO YA UTAFITI 3
4.0. JUMLA YA WASHIRIKI KWA KILA MKOA 4
5.0. MAELEZO YA MBINU ZA UTAFITI 5
7.0. MATOKEO YA UTAFITI 7
8.0. MAONI JUU YA KIONGOZI ANAYEFAA KUWA RAISI , 2015 14
9.0. CHAMA CHA SIASA CHENYE MVUTO NA KUKUBALIKA KWA WANANCHI 19
10.0. SIFA ZA WASHIRIKI WA UTAFITI 22
11.0. IDADI YA KURA ALIZOPIGIWA MWANASIASA MASHUHURI KWA KILA MKOA 24
12. KIGEZO CHA ELIMU NA JINSI WALIVYOPIGA KURA 26
13. KIGEZO CHA UMRI NA JINSI WALIVYOPIGA KURA 27
14. HITIMISHO 28
VIAMBATANISHO 30

Vielelezo Katika Jedwali

Jedwali Na.1 : Majina ya Wanasiasa Mashuhuri Nchini Tanzania..... v
Jedwali Na 2.Washiriki kwa kila mkoa, Tanzania bara..... 4
Jedwali Na. 3 : Ushiriki wa Chama na Kura zilizopigwa..... 7
Jedwali Na 4: Vyama Vingine Vya Siasa 7
Jedwali Na.5 : Washiriki kwa kila mkoa, Tanzania bara..... 8
Jedwali Na. 6: Vipaumbele vya Kumchagua Raisi atakayefaa kwa mwaka 2015..... 9
Jedwali Na. 7: Sifa na Vigezo vya Raisi atakayefaa kuchaguli kwa mwaka 2015..... 10
Jedwali Na. 8: Sifa na Vigezo vya Mbunge atakayefaa,2015..... 12
Jedwali Na. 9: Sifa na Vigezo vya Diwani atakayefaa,2015..... 13
Jedwali Na. 10: Mwanasiasa Anayefaa kuwa Raisi,2015..... 16
Jedwali Na. 11: Kura Kulingana na Itikadi ya Vyama kwa Wanasiasa..... 18
Jedwali Na. 12: Chama cha siasa chenye Mvuto nchini..... 19
Jedwali Na. 13: Mtawanyiko wa kura kwa Chama Chenye Mvuto..... 21
Jedwali Na. 14: Kiwango Cha Elimu ya Washiriki..... 22
Jedwali Na. 15: Umri wa Washiriki..... 23
Jedwali Na. 16: Idadi ya Kura Ki-Mkoa kwa Kila Mwanasiasa 25
Jedwali Na. 17: Kigezo cha Elimu walivyopiga na kura kwa wanasiasa watatu wa kwanza..26
Jedwali Na. 18: Kigezo cha Elimu walivyopiga na kura kwa wanasiasa watatu wa kwanza.27

SHUKRANI

*Utafiti huu umefanywa na taasisi isiyo ya kiserikali inayojukana kwa jina, "**Positive Thinkers Tanzania**". Kwa niaba ya Positive Thinkers Tanzania, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki kufanikisha zoezi la utafiti huu. Napenda kuwashukuru washiriki wa utafiti kutoka mikoa yote Tanzania bara waliokubali kushiriki na kutoa maoni yao katika dodoso la utafiti. Pia napenda kuwashukuru watafiti wasaidizi waliojitolea kwenda mikoani kuongea na wadau ambao pamoja na changamoto walizokumbana nazo wameweza kuleta matokeo mazuri ya utafiti.*

*Pia napenda kuchukua nafasi hii ya pekee kumshukuru ndugu **Fasili Boniphace**, mtaalamu na mshauri maswala ya maendeleo, miradi, uongozi,biashara na Ujasiriamali kutoka kampuni ya **EBI Consulting Limited (www.theidea.biz)** kwa kuandaa ripoti hii ya utafiti kwa umahiri na weredi mkubwa.Pamoja na mambo mengine, ndugu Fasili Boniphace amekuwa mshauri wa karibu sana wa taasisi ya Positive Thinkers Tanzania; tunamshukuru kwa moyo wa kujitolea alioonyesha katika zoezi hili la utafiti.*

Isingekuwa rahisi kutimiza madhumuni ya utafiti huu bila ushirikiano na serikali, hasa viongozi wa serikali husika katika mikoa ambapo watafiti walifika. Ninapenda kuwashukuru viongozi wa serikali za mitaa, kata, wilaya na mikoa popote pale ambapo watafiti walipita kupata ushirikiano wao. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania. Jumla ya mikoa 13 Tanzania bara ilishiriki utafiti huu ambapo jumla ya washriki 3298 walishiriki kutoa maoni yao katika dodoso la utafiti.

*Positive Thinkers Tanzania inapenda kuchukua nafasi ya pekee kumshukuru madhamini wa utafiti huu ambaye ni **Invesol Group (T) Limited** ; ambao ni wataalamu wa kuunda mifumo ya kompyuta. Pamoja na hayo, tunapenda kuwashukuru wajumbe wa PTT (Premier Members)kwa michango yao ya hali na mali kwa kufanikisha michango 30% ya gharama za kufanya utafiti.*

Positive Thnkers Tanzania, inayo imani kuwa, matokeo ya utafiti huu ni mwongozo muafaka kwa ajili ya wadau wote nchini katika maswala ya siasa na maendeleo. Utafiti umebaini mambo mengi ya msingi ambayo wanasiasa na wanaharakati wa maendeleo wanahitaji kuyatazama kwa mtazamo mpya na makini, kuzingatia na kuwa wabunifu hasa katika kipindi ambacho wananchi wana uelewa mkubwa juu ya mambo ya msingi yanayoathiri hatima ya maendeleo na mafanikio ya nchi yao. Kwa mfano, maswala ya ufisadi na uadilifu wa viongozi yamekuwa mambo ya msingi kama sifa na vigezo vya kumchagua kiongozi. Wananchi (wapiga kura) wanavyo vigezo vya kumchagua kiongozi anayefaa bila kujali itikadi ya chama. Hata hivyo, wapo wananchi wengi ambao wameonesha nia na uwezo wa kuamua hatima maendeleo ya nchi yao bila kuwa katika misingi ya chama chochote.

Kwa niaba ya Positive Thinkers Tanzania, ninawashukuru nyote kwa ushiriki wenu na kuwaomba usomaji mwema wa ripoti hii.

Tibatizibwa Gulayi Yabutinga
Raisi, Positive Thinkers Tanzania

MUHTASARI WA UTAFITI

Utafiti huu umetokana na hamasa ya muono chanya wa wajumbe wa PTT na wadau wengine wa maendeleo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na teknolojia kutaka kujua hali halisi ya mtazamo, vigezo na matarajio ya wananchina katika kumchagua kiongozi wao. Kutokana na tafiti mbali mbali zilizofanyika nchini Tanzania katika maswala ya ushiriki wa wananchi kufanya maamuzi ya kisiasa; swala la vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kumchagua kiongozi limekuwa halipewi nafasi kubwa. Kutokana na changamoto nyingi zinazojitokeza, hasa kipindi hiki ambacho Tanzania inajiandaa kufanya uchaguzi mkuu kitaifa, shirika lisili la kiserikali la **Positive Thinkers Tanzania** (PTT) liliamua kufanya utafiti juu ya vigezo, sifa na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kumchagua kiongozi.

Lengo kuu la ufatifi huu lilikuwa ni **"Kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania".** Maswali ya msingi yaliyoongoza utafiti huu ni pamoja na yafuatayo:

i. Je, ni vigezo gani wananchi wanavyovijua vinavyowaongoza kufanya maamuzi ya kuchagua kiongozi wanayemtaka kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 nchini Tanzania.
ii. Je, ni matarajio gani waliyonayo wananchi kwa kiongozi watakaye mchagua kuongoza kwa ngazi ya Diwani, Mbunge na Raisi?
iii. Je, chama gani kina mvuto wa kuongoza nchi kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 nchini Tanzania?
iv. Je, ni kiongozi (Mwanasiaisa) gani anayeonesha anafaa kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?
v. Je, vipaumbele gani wananchi wanatarajia vitimizwe na kiongozi atakayefaa kuwa Raisi wa awamu ya tano?
vi. Je, kiwango gani cha elimu na umri wa wapiga kura wanaotambua umuhimu wa kuchagua kiongozi, na maoni gani waliyonayo juu ya vigezo vya kuchagua kiongozi?

Jumla ya mikoa 13 Tanzania bara ilishiriki utafiti huu ambapo jumla ya washriki 3298 walishiriki kutoa maoni yao katika dodoso la utafiti. Mbinu kuu za utafiti zilikuwa ni dodoso (Questionnaire) na mahojiano (interviews).

Utafiti ulishirikisha matabaka mbali mbali ya washiriki kwa misingi ya elimu na umri, itikadi za chama na wasio na itikadi ya chama chochote. Washiriki walipatikana kwa njia ya "*Random Sampling*",yaani, pasipo ushawishi wa awali au kupanga nao muda wa kukutana. Hii ni njia ya papo kwa hapo ambapo mshiriki alitoa maoni yake bila ushawishi wa mtu mwingine. Utafiti ulihusisha vijana, watu wazima na wazee.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini mambo mengi ya msingi ambayo wananchi, watawala, wadau wa maendeleo na wanasiasa kwa pamoja wanahitaji kuyajua na kuyafanyia kazi ili kuifikisha nchi katika hatima nzuri ya maendeleo ya jamii na uchumi kwa ujumla. Pamoja na mambo mengine, utafiti ulilenga ngazi muhimu za uongozi wa kisiasa, ambazo ni: *Diwani, Mbunge na Raisi*. Nafasi hizi zilikuwa za muhimu kulingana na mazingira ya siasa nchini Tanzania.

Katika ngazi ya Uraisi, jumla ya majina 15 ya wanasiasa mashuhuri nchini yalipendekezwa ili yapigiwe kura katika misingi mwanasiasa mwenye mvuto kwa wananchi na chama chenye mvuto kulingana na vigezo vya kumchagua kiongozi wanayemtarajia.

Jedwali Na. 1: Wanasiasa Mashuhuri Nchini Tanzania.

Na.	Jina la Kiongozi	Wadhifa/ Sifa ya Kiongozi
1	Mh. Edward N. Lowassa	Waziri Mkuu Mstaafu na Mbunge wa Monduli,CCM
2	Mh. Wilbrod Slaa	Katibu Mkuu Taifa- CHADEMA
3	Mh. Mwigulu Nchemba	Naibu Waziri wa Fedha na Naibu Katibu Mkuu Taifa-CCM
4	Mh. Ibrahimu Lipumba	Mwenyekiti Taifa -CUF
5	Mh. Zitto Kabwe	Mbunge, CHADEMA
6	Mh. John P. Magufuli	Waziri, Wizara ya Ujenzi,CCM
7	Mh. Bernard Membe	Waziri wa Mambo ya Nje, CCM
8	Mh. Mizengo Pinda	Waziri Mkuu, CCM
9	Mh. January Makamba	Naibu Waziri, Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Mbunge Bumbuli,CCM.
10	Mh. Mark Mwandosya	Waziri asiye na Wizara Maalum
11	Mh. James Mbatia	Mwenyeki- Taifa, NCCR-Mageuzi
12	Mh. Hussein Mwinyi	Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
13	Mh. Steven Wassira	Waziri wa Kilimo
14	Mh. Fredrick Sumaye	Waziri Mkuu Mstaafu, CCM
15	Mh. Samwel Sitta	Waziri wa Uchukuzi

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Muhtasari wa Matokeo Makuu ya Utafiti yalikuwa kama ifuatavyo:

a) Idadi ya mikoa iliyoshiriki utafiti Tanzania bara ilikuwa 13; ambayo ni: Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Tanga, Lindi, Dodoma, Pwani, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga na Morogoro(Pamoja na Wilaya zake na baadhi ya vijiji, kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na.2

b) Katika ushiriki wa vyama vikuu 4 vya siasa, kura zilizopigwa ni kama ifuatavyo: CCM (1144), CHADEMA(1117), CUF (360) na NCCR-Mageuzi (77) na Vyama vingine vya siasa asilimia 19 ya kura zote.

c) Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, idadi kubwa ya kura za washiriki zilipatikana katika mikoa ya Dar es Salaam (26.8%), Arusha (9.9%), Mwanza (9.2%), na Mbeya (7.2%). Mikoa mingine ilikuwa na washiriki wachache. Takwimu za mikoa mingine ipo kwenye jedwali Na. 2.

d) Vipaumbele vikuu vya Raisi anavyotakiwa kuanza navyo ni pamoja na: Kuthibiti rusha na ufisadi (33.3%), ajira (20.2%), elimu (16.6%), huduma za afya (12%) na kilimo (3.9%).

e) Kuhusu sifa na vigezo vikuu vya kumchagua **Raisi** ni pamoja na : Utendaji bora kwa vitendo (49%), uadilifu (33.5%), umri na uzoefu kazini (7.7%), na elimu bora (6%).

f) Sifa na vigezo vya kumchagua kiongozi anayefaa kuwa **Mbunge** ni pamoja na utendaji bora kwa vitendo (48.4%), uadilifu (35.6%), uzoefu kazini (6.4%), na elimu nzuri (4.9%).

g) Sifa na vigezo vya kumchagua kiongozi anayefaa kuwa Diwani ni pampja na vifuatavyo: utendaji bora kwa vitendo (44.7%), uadilifu (37.1%), uzoefu kazini (7.4%) na elimu bora (6%).

h) Idadi ya kura za washiriki juu ya kiongozi (Mwanasiasa) anayefaa kuwa Raisi ni kama ifuatavyo: Mh. Edward Lowassa (22.8%), Mh. Wilbrod Slaa (19.5%), Mh. Mwigulu Nchemba (10.6%), Mh. Ibrahimu Lipumba (8.9%), Mh. John Magufuli (6.8%), Mh. Zitto Kabwe (6.7%), Mh. Bernard Membe (5.9%), Mh.Mizengo Pinda (3.2%), Mh. Samwel Sitta

(2.2%), Mh. January Makamba (1.6%), Mh. Mark Mwandosya (1.2%), Mh. James Mbatia (1%), Mh. Hussein Mwinyi (0.9%), Mh. Steven Wassira (0.4%), na Mh. Fredrick Sumaye (0.3%)

i) Kutokana na matokeo ya utafiti, Jedwali Na. 11 hapo chini linaonesha kuwa kura washiriki walipiga kura siyo tu kwa kujali itikadi na mapenzi ya vyama vyao, bali utashi na vigezo vya kumchagua kiongozi ndiyo ilikuwa msimamo wao. Ndiyo maana, katika jedwali Na. 11 inaonesha kuwa washiriki kutoka vyama tofauti vya siasa waliwapendekeza viongozi wasio wa vyama vyao vya siasa. Pamoja na hayo, wapo wengine wasiokuwa na vyama vya siasa lakini walipendekeza kulingana na sifa za mwanasiasa.

j) Kuhusu "**chama chenye mvuto"** kwa wananchi, utafiti umebaini kuwa vipo vyama vitatu vya siasa nchini ambavyo ndivyo vimeonekana kuwa na mvuto mkubwa (vinakubalika na wananchi kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu). Chama kilichoongoza kwa mvuto ni **CHADEMA (44.6%),** kikifuatiwa na **CCM (34.4%)**. Nafasi ya tatu kwa mvuto ilichukuliwa na Chama Cha Wananchi **(CUF: 10.6%).** Vyama vingine vya siasa vilikuwa na uwakilishi mdogo wa kura.

k) Kutokana na kigezo cha elimu ya washiriki, utafiti umebaini kuwa idadi kubwa ya washiriki wa utafiti walikuwa na elimu ya sekondari (33.7%) wakifuatia wenye elimu ya shule ya msingi (29.7%). Kwa walio na elimu ya cheti/ stashahada walikuwa (8.5%). Wakati huo, wenye elimu ya chuo kikuu walikuwa (12.8%).

l) Kuhusu umri wa washiriki wa utafiti, washiriki wa umri kati ya 18-24 walikuwa 20.9%, wenye umri wa miaka 25-34 walikuwa (29.5%), na wenye umri kati ya 35-44 walikuwa (24.9%). Kwa upande mwingine, washiriki wa umri kati ya miaka 45-60 walikuwa (17.1%) na wenye umri zaidi ya 60 walikuwa (7.6%).

1.0. UTANGULIZI

Tangu kuanza kwa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini Tanzania katika miaka ya 1992; ukuaji wa demokrasia nchini Tanzania umeendelea kuleta mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha ya wananchi. Mfano: mabadiliko ya kifikra kutoka chama kimoja (Chama Cha Mapinduzi) hadi mfumo wa vyama vingi vya siasa, kiuchumi, kisiasa, kijamii, kimila, utawala bora, uhuru wa kuchagua na kujieleza, usawa, haki pamoja na sheria na kanuni mbali mbali.

Mabadiliko mengine ni pamoja na mfumo wa uchumi unaotegemea ukuaji wa sekta binafsi, na mwamko mkubwa wa ushiriki wa wananchi katika kuamua hatima za maisha yao kupitia mfumo wa siasa, viongozi wanaowachagua na uwajibikaji wa watumishi wa sekta ya umma. Hii inamaanisha kuwa fikra na mitazamo ya watanzania wa mwaka 2015 siyo zile za mwaka 1990 au 1980. Tafiti na tathimini mbali mbali zilizofanyika hapo awali nchini Tanzania juu ya hali ya ushiriki wa wananchi katika kufanya maamuzi ya maswala ya kisiasa na uchumi zinaonesha kuwa kuna mwamko mkubwa wa wananchi kuhoji na kutaka kujua hatima ya maendeleo. Wananchi wanahoji nani atakuwa kiongozi atakayefaa kuwa raisi wa nchi, mbunge, diwani, mjumbe wa serikali za mitaa, n.k.

Wananchi wanahoji: Je, nchi yetu itakuwa katika mikono ya viongozi waadilifu na wawajibikaji? Je, misingi gani ya uongozi itakayolifikisha taifa la Tanzania katika hatima wanayoitaka wananchi?. Mawasli haya na mengineyo yamepelekea kuwepo na haja ya kufanya utafiti juu ya vigezo wanavyovitarajia wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu nchini Tanzania ifikapo Oktoba 2015. Hili pengine linadhihirishwa na mwamko mkubwa wa kizazi kipya cha vijana kutafuta uongozi katika vyama vya siasa, na msukumo wa kutaka taifa liongozwe na vijana badala ya wazee kama ilivyozoeleka katika miongo iliyopita.

Pamoja na mambo yote; swali kubwa ni kwamba: Je, wananchi wanajua wanachokitarajia na wanachohitaji kutoka kwa viongozi watakao wachagua? Je, ni vigezo gani wananchi wanatarajia kuvitumia ili kufanya maamuzi ya kumchagua kiongozi wanayemtaka?

Kutokana na changamoto za maisha zinazowakabili wananchi kiuchumi, kisiasa, kijamii; na mahitaji waliyonayo wananchi; imepelekea taasisi ya **"Positive Thinkers Tanzania"**[1] kufanya utafiti huu ili kubaini mahitaji ya wananchi, matarajio yao kwa viongozi watakao wachagua na

[1] Shirika lisilo la kiserikali lenye makao makuu Dar es Salaam.

vigezo wanavyotumia kufanya maamuzi ya kumchagua kiongozi katika ngazi ya Diwani, Mbunge na Raisi.

Katika utafiti huu, jumla ya mikoa 13 ilishiriki katika utafiti; ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Tanga, Lindi, Dodoma, Pwani, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga na Morogoro. Jumla ya washirki 3298 kutoka mikoa iliyotajwa walipata nafasi ya kutoa maoni yao katika utafiti huu.

Pia katika utafiti huu, jumla ya viongozi 15 wa vyama vya siasa na serikali walioko madarakani na wastaafu walipigiwa kura kupitia dodoso zilizopelekwa kwa wananchi walioshiriki katika utafiti kwa vigezo vya kiongozi mwenye mvuto na mwenye sifa za kuwa raisi wa Tanzania. Viongozi waliopigiwa kura ni pamoja na waliooneshwa kwa majina katika chati hapa chini.

2.0. MAELEZO YA POSITIVE THINKERS TANZANIA

Positive Thinkers Tanzania(PTT), ni taasisi isiyokuwa ya kiserikali iliyosajiriwa nchini Tanzania tarehe 1 Februari 2011. Positive Thinkers Tanzania ilisajiliwa kwa nambari 00004344. Makao makuu ya PTT yako Dar es Salaam, Tanzania.

Taasisi ya PTT imeundwa na watanzania wenye mtazamo wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Positive Thinkers Tanzania inaamini kuwa mtu akijengewa hali ya kuwa na mtazamo chanya ataweza kufanya mabadiliko kutoka hali duni na kuwa na maisha bora. Pia mtu akiwa na mtazamo chanya anaweza kuwajibika na kuleta mabadiliko yanayohusu hatima yake ya sasa na ya baadaye. PTT inaamini kuwa jamii ya watanzania inaweza kufanya maamuzi chanya juu ya hatima ya mtu binafsi, mtaa, mkoa na hata taifa kwa ujumla.

2.1. Dira ya PTT:

Kuwa taasisi inayoongoza kuelimisha, kujenga uwezo na ubunifu kwa jamii ya watanzania, kujenga mtazamo chanya katika harakati za kutatua changamoto zinazoikabili jamii ya kitanzania.

2.2. Dhamira ya PTT

Positive Thinkers Tanzania inaamini katika kujenga uwezo na fikra chanya kwa wadau na raia, kujenga uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, kutafiti na kutathimini matarajio na mahitaji ya wananchi juu ya mustakabali na hatima zao, pamoja na kushiriki katika kutatua changamoto za maendeleo ya uchumi, jamii na siasa nchini.

3.0. MELEZO YA UTAFITI

3.1. Kwa nini Utafiti huu umefanyika?

Wazo la utafiti huu limeanzishwa na kutekelezwa na taasisi ya Positive Thinkers Tanzania(PTT). Utafiti huu umefanyika mwezi Februari hadi Machi 2015, na kushirikisha mikoa 13 ya Tanzania bara. Mikoa hii ni pamoja na Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Tanga, Lindi, Dodoma, Pwani, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga na Morogoro. Katika utafiti huu, PTT ilitumia maswali ya msingi kuibua hoja na maoni ya wananchi juu ya vigezo vya kumchagua kiongozi, matarajio, hatima na maslahi ya nchi ambayo wapiga kura wanatumia kumchagua kiongozi wanaye mtaka.

3.1. Maswali ya Utafiti

Maswali ya msingi yaliyoongoza utafiti huu ni pamoja na yafuatayo:

a) Je, ni vigezo gani wananchi wanavyovijua vinavyowaongoza kufanya maamuzi ya kuchagua kiongozi wanayemtaka kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 nchini Tanzania.
b) Je, ni matarajio gani waliyonayo wananchi kwa kiongozi watakaye mchagua kuongoza kwa ngazi ya Diwani, Mbunge na Raisi?
c) Je, chama gani kina mvuto wa kuongoza nchi kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 nchini Tanzania?
d) Je, ni kiongozi gani anayeonesha anafaa kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?
e) Je, vipaumbele gani wananchi wanatarajia vitimizwe na kiongozi anayefaa kuwa Raisi?
f) Je, kiwango gani cha elimu ya wapiga kura waliotoa maoni na vigezo vya kuchagua kiongozi?

3.2. Lengo Kuu La Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania.

3.3. Malengo Mahsusi ya Utafiti

Malengo mahususi ya utafiti yalikuwa ni kama ifuatavyo:

a) Kutambua vigezo wanavyotumia wananchi kufanya maamuzi, kupiga kura na kuchagua kiongozi.
b) Kutathimi matarajio ya wananchi kwa kiongozi watakaye mchagua kuwa Diwani, Mbunge au Raisi.
c) Kutathimi chama cha siasa chenye mvuto wa kuongoza nchi.

d) Kutathimini kiongozi mwenye mvuto anayefaa kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

e) Kutambua vipaumbele vya wananchi wanavyotarajia kupima kiongozi anayefaa kuwa Raisi.

f) Kubaini kiwango gani cha elimu ya wapiga kura waliotoa maoni na vigezo vya kuchagua viongozi.

4.0. JUMLA YA WASHIRIKI KWA KILA MKOA

Jumla ya washiriki 3298 kutoka mikoa 13 Tanzania bara walipata nafasi ya kushirki katika utafiti huu. Washiriki wa utafiti walipatikana maeneo ya mijini na vijini, wafanyakazi na wakulima, vijana na wazee, wa kike na wa kiume. Maelezo zaid ya maeneo ya washirki yameoneshwa katika Jedwali Na. 2 hapo chini.

4.1. Idadi ya Washiriki Ki-Mkoa

Chati inayoonesha washirki kwa kila mkoa, Tanzania bara.

JedwaliNa.2 :Washiriki kwa kila mkoa, Tanzania bara.

Na.	Mkoa	WILAYA/VIJIJI/MITAA NA VITONGOJI	Idadiyawashiriki
1	Dar es Salaam	ILALA,TEMEKE,KINONDONI,Kigamboni, Kariakoo,YomboVituka, Masaki, Chanika, Buguruni,Tabata, Sinza, Mliman City, Tegeta, Tandika, UbungonaUbungo stand, Kimara, Kibamba, Mwananyamala,Makumbusho, Kijitonyama, Mbagalarangitatu, Bunju, Boko, Mikocheni	885
2	Arusha	Arusha mjini,Soweto, Kiloleni, Sanawari, Ungalimited, Sakei,kisongo, Ngarinaro, Ngiro, Karatumjini, mbumbulu,Mondulimjini, mtowambu ,mondulijuu. Longido(Namanga, Tingatinga), Meru (USA River, Tengeru, Majiya chai, Katiti	325
3	Mwanza	Nyamagana,Ilemela,Sengerema,Misungwi na Magu,	302
4	Mbeya	Mbeya mjini,Tunduma,Mbozi,Tukuyu, Rungwe, Kyela,	238
5	Mtwara	MTWARA MJINI,Mikindani,Mashujaa, Stendkuu, Sabasaba, Shangai, Chuo cha utumishi, SAUT. KIANGO,KUKUTA,LIGALA,HURIA,VIERA,NAFU, Magomeni,Chikongola.	214
6	Tanga	Segera, Korogwe, Muheza, Tanga mjini, na Maeneo yaliyo karibu na mji wa Tanga.	208
7	Lindi	Lindi Mjini, Stendi Kuu,Balewa, Soko Kuu, Saba saba, Ndolo, Mitaa ya Benki na Bliji. Santolini,Muhimbili, Mikumbi, Mtanda,Kariakoo,Chelene, Mchunda na Maeneo ya vijiji vya karibu na Lindi mjini.	207
8	Dodoma	Dodoma Mjini, Kongwa na Msalato	202
9	Pwani	Kibaha, Malandizi, Chalinze, Msata	199
10	Iringa	IRINGA mjini, Mafinga, Mufindi	195
11	Kilimanjaro	Moshi mjini (Majengo,Pasua, Kibororoni, Msaranga. HAI	195

		mjini, KIA, Rombo,Mwanga, Same Mjini, kijiji cha Masandale.	
12	Shinyanga	Shinyanga Mjini na maeneo ya vijiji vya karibu na mji.	126
13	Morogoro	Utafiti ulifanyika kwa simu	2
JumlayaWashirikikati kamikoa 13 iliyoshiriki			**3298**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

5.0. MAELEZO YA MBINU ZA UTAFITI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania. Katika utafiti huu ulifanyika katika mikoa 13 ya Tanzania bara. Makundi matatu ya viongozi wa kisiasa yalihusishwa katika kupata maoni ya wananchi juu ya viongozi wanafaa. Makundi hayo ni katika nafasi ya *"Diwani, Mbunge na Raisi"*. Mbinu kuu mbili za utafiti zilitumika ili kupata majibu ya maswali kutoka kwenye sampuli za washiriki wa utafiti. Mbinu hizo ni dodoso na mahojiano kwa simu. Katika utafiti huu, sampuli ya washiriki 3298 walihusika katika utafiti. Kati yao, washirki 3281 walishiriki kwa njia ya dodoso, na washiriki 17 walishiriki kwa njia ya mahojiano kwa simu.

5.1. Dodoso la Utafiti

Dodoso (questionnaire) la utafiti lilitumika kupata maoni ya washirki. Jumla ya washiriki 3281 walishiriki kwa njia ya dodoso, na 17 walishiriki kwa njia ya mahojiano ya simu (telephone interviews). Dodoso la utafiti liliundwa na taasisi ya Positive Thinkers Tanzania(PTT). Dodoso hili lilitengenezwa kwa njia rahisi ili kurahisisha mawasiliano kati ya watafiti na washiriki wa utafiti.

Dodoso la utafiti lilibeba maswali 7 ya msingi ambayo yaliyohoji mambo yafuatayo:

i. Umri, elimu na itikadi ya chama ya mshiriki
ii. Chama cha siasa chenye mvuto na kukubalika kwa wananchi
iii. Kiongozi atakayefaa kuwa Raisi katika uchaguzi mkuu wa 2015 nchini Tanzania.
iv. Sifa na vigezo vya kiongozi anayefaa kuwa Raisi wa Tanzania 2015
v. Vipaumbele vya Raisi kwa matarajio ya wananchi
vi. Sifa na vigezo vya kiongozi atakaye faa kuwa Diwani,
vii. Sifa na vigezo vya kiongozi atakayefaa kuwa Mbunge kwa mwaka 2015.

5.2. Mfumo wa Ushiriki katika Dodoso

Dodoso la utafiti lilijazwa kwa mfumo wa mazungumzo ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mshiriki(Respondent). Mtafiti aliuza swali na mshiriki alijibu kwa kufuate vipengele vilivyokuwepo kwenye dodoso. Maelezo zaidi kuhusu dodoso yanapatikana kama kiambatanisho Na. 1, mwisho wa ripoti hii.

5.3. Mahojiano kwa Simu

Baadhi ya washiriki wa utafiti walitoa maoni yao kupitia mahojiano yaliyo fanyika kwa njia ya simu. Jumla ya washiriki 17 walitoa maoni kwa njia ya simu.

5.4. Uchambuzi wa Sampuli kwa Mfumo wa Elektroniki

Ili kurahisisha utaratibu wa kuchuja sampuli na kuainisha majibu yaliyotolewa na washiriki, watafiti walipewa mafunzo kabla ya kuanza utafiti namna ya kuingiza taarifa za utafiti kwa mfumo wa kielektroniki unaojulikana kwa jina la ***"PTT Research Data Application"***[2] ulioruhusu kuona bayana hali halisi ya matokeo ya utafiti mahala popote kila mtafiti anapoingiza majibu.

5.5. Washirki kwa Msingi ya Jinsia

Katika utafiti huu, jumla ya washiriki walikuwa 3298; kati yao asilimia 42 walikuwa ni washiriki wa kike na asilimia 58 walikuwa washiriki wa kiume.

5.6. Jinsi Washiriki walivyopatikana

Watafiti wasaidizi walienda katika mikoa waliyopangiwa; washirki walipatikana kwa mfumo wa "Random Sampling"; yaani, pasipo kuwepo mawasiliano ya awali, bila ushawishi. Watafiti walienda maeneo ya utafiti na kukutana na wananchi kadri walivyokuwa wakikutana nao maeneo yao.

6.0. VYAMA VISHIRIKI NA KURA ZILIZOPIGWA

6.1. Vyama Vilivyopigiwa Kura kwa wingi.

Utafiti ulihusisha ushiriki wa vyama vyote vya saisa. Vikiwemo vyama vikuu vinne (4) vya siasa nchini. Jedwali lifuatalo linaonesha jumla ya washirki kwa kila chama kilichoshiriki.

[2] Mfumo wa elektroniki uliobuniwa na watafiti wa sayansi ya komputa katika taasisi ya Positive Thinkers Tanzania.

Jedwali Na. 3 : Ushiriki wa Chama na Kura zilizopigwa

Na.	Chama	Idadi ya Kura	Asilimia (%)
1	Chama Cha Mapinduzi (CCM)	1144	34.68
2	Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)	1117	33.86
3	Civic United Front (CUF)	360	10.91
4	NCCR - Mageuzi	77	2.33

Chanzo: Utafiti, PTT 2015

Jedwali Na 4: Vyama Vingine Vya Siasa (19%)

Na.	Vya Vya Siasa
5	Alliance For Change and Transparency (ACT-Tanzania)
6	Tanzania Labour Party (TLP)
7	The United Democratic Party (UDP)
8	Chama Cha Haki na Ustawi (CHAUSTA
9	Progressive Party of Tanzania (PPT- Maendeleo)
10	Sauti ya Umma (SAU)
11	Jahazi Asilia (JAHAZI ASILIA)
12	Alliance for Tanzanian Farmers Party (AFP)
13	Demokrasia Makini (MAKINI)
14	United People's Democratic Party (UPDP)
15	National Reconstruction Alliance (NRA)
16	Democratic Party (DP)
17	Tanzania Democratic Alliance (TADEA)
18	The Union for Multiparty Democracy(UMD) of Tanzania
19	National League for Democracy (NLD)

Chanzo: Utafiti, PTT 2015

7.0. MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii ya ripoti ya utafiti inaainisha matokeo ya utafiti kwa kuzingatia maswali ya msingi na malengo mahususi ya utafiti uliofanywa na taasisi ya Positive Thinkers Tanzania. Jumla ya maswali 7 ya msingi yaliandaliwa kwenye dodoso la utafiti. Kila swali liligawanywa katika vipengele ili kurahisisha utoaji wa taarifa na majibu yaliyotarajiwa. Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania. Hivyo, matokeo ya utafiti huu yanatoa mwelekeo wa matarajio na vigezo vya kuchagua viongozi. Kwa mfano, katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba 2015, wananchi, wapiga kura wana maoni gani kuhusu vyama vinavyoonesha mwelekeo wa kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi, na viongozi wanaoonesha nia ya kuwa viongozi.

7.1. Washiriki Ki-Mkoa

Jedwali Na.5 : Washiriki kwa kila mkoa, Tanzania bara.

Na.	Mkoa	Idadi ya washiriki	Asilimia (%)
1	Dar es Salaam	885	26.8
2	Arusha	325	9.9
3	Mwanza	302	9.2
4	Mbeya	238	7.2
5	Mtwara	214	6.5
6	Tanga	208	6.3
7	Lindi	207	6.27
8	Dodoma	202	6.1
9	Pwani	199	6.03
10	Iringa	195	5.9
11	Kilimanjaro	195	5.9
12	Shinyanga	126	3.8
13	Morogoro	2	0.06
Jumla ya Washiriki katika mikoa 13 iliyoshiriki		**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Kutokana na takwimu katika jedwali nambari 5 hapo juu, jumla ya mikoa 4 ilikuwa na ushiriki mkubwa. Kwa mfano: Dar es Salaam ilikuwa na washiriki 885 (26.8%), Arusha 325 (9.9%), Mwanza 302 (9.2%) na Mbeya ilikuwa na washiriki 238 (7.2%).

7.2. Sifa, Vigezo na Vipaumbele Vya kumchagua Kiongozi anayefaa 2015

Utafiti ulilenga kujua endapo kuna vipaumbele ambavyo wananchi wanavifahamu na endapo wanaweza kuvitumia kumchagua kiongozi. Katika utafiti huu, nafasi tatu za uongozi wa siasa zilihusishwa ambazo ni *Raisi, Mbunge na Diwani*. Kila nafasi ilikuwa na swali maalumu lililohoji uelewa wa wananchi juu ya vigezo na vipaumbele wanavyotumia kumchagua kiongozi wanayemtaka.

7.2.1. Vipaumbele vya Kumchagua Raisi

Swali nambari 5 katika dodoso lilihoji juu ya vipaumbele ambavyo Raisi ajaye anatakiwa aanze navyo kama kero kuu zinazorudisha nyuma maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Dodoso la utafiti lilikuwa na vidokezo vya vipaumbele 9; ambavyo washiriki wa utafiti waliombwa kuviainisha na kuvichagua. Katika swali hilo, vidokezo vya vipaumbele vya kumchagua Raisi vilikuwa ni: Barabara bora, upatikanaji wa maji safi na salama, huduma za afya(hospitali), elimu, umeme, ajira, kilimo, kudhibiti rushwa, kudhibiti ufisadi, na vinginevyo. Matokeo ya kura za vipaumbele vilikuwa kama inavyoneshwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 6: Vipaumbele vya Kumchagua Raisi atakayefaa kwa mwaka 2015

Na.	Vipaumbele Vya Kumchagua Raisi	Kura zilizopigwa	Asilimia(%)
1	Kudhibiti Rushwa na Ufisadi	1097	33.26
2	Ajira	667	20.22
3	Elimu	546	16.55
4	Hospitali (Huduma za afya)	395	11.97
5	Maji	233	7.1
6	Barabara	142	4.3
7	Kilimo	131	3.97
8	Umeme	40	1.21
9	Vinginevyo	47	1.42
Jumla ya Kura zilizopigwa		**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Kutokana na kura zilizopigwa, kipaumbele kikuu cha kumchagua Raisi kimeonekana kuwa ni Kudhibiti rushwa na ufisadi ambapo jumla ya kura **1097 (33.26%)** zilipigwa. Hii inamaanisha kuwa, wananchi (wapiga kura) wanaufahamu mkubwa juu ya maslahi ya nchi yao hasa ikizingatiwa swala la maslahi ya rasilimali za nchi na hatima ya maendeleo yao. Wananchi wamechoshwa na rushwa na ufisadi uliokithiri unaotendwa na watumishi wa umma na wanasiasa. Katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, wananchi wako makini kumchagua raisi mwenye nia halisi ya thabiti,

kuondoa na kukomesha rushwa nchini. Pamoja na mambo mengine, swala la ajira limechugua nafasi kubwa sana. Jumla ya kura **667 (20.22%)** zilipigwa kuonesha kuwa tatizo la ajira ni kubwa sana nchini, hasa upande wa vijana walio na elimu nzuri lakini hawana ajira. Hili lina tafasiri nyingi: moja ni kuwa ukosefu wa ajira unasababisha matumizi hafifu ya rasilimali watu; pili. ukosefu wa ajira ni janga la taifa. Tatizo la ajira nchini, hasa kwa vijana ni janga kuu linalosababisha matumizi mabaya ya nguvu kazi na rasilimali watu. Ukilinganisha na vipaumbele vinginevyo, maswala matatu yamechukua nafasi kubwa kama vigezo vikuu vya kumchagua Raisi wa nchi; ambavyo ni "***Kudhibiti rushwa na ufisadi, ajira na elimu"*.** Hivyo, Raisi atakayechaguliwa anatarajiwa kutoa majibu ya hizi changamoto.

Upande mwingine, huduma za afya kama hospitali na matibabu zimechugua 11.97%. Huduma ya maji 7.1%, barabara 4.3%, kilimo 3.97% na umeme 1.21%. Swali la kujiuliza hapa ni kuwa: ***Kwa nini huduma za msingi kama barabara, umeme, maji na afya zimechukua nafasi ndogo?*** Hili linaweza kuwa na tafsiri kuwa wananchi wanachukua tahadhari ya mambo yanayoweza kuharibu hatima ya maendeleo ya nchi. Kwa mfano, ufisadi wa mabilioni ya fedha za umma uliopo katika utumishi wa umma, elimu ambayo ni ufunguo wa maisha na afya ambayo ni msingi wa maendeleo ya rasilimali watu.

7.2.2. Sifa na Vigezo vya kiongozi anayefaa kuwa Raisi 2015

Utafiti ulilenga kujua endapo kuna sifa na vigezo vya kiongozi watakayemchagua kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2015. Swali Na. 4 katika dodoso la utafiti lilihoji juu ya sifa na vigezo vya kiongozi anayefaa kuwa Raisi katika uchaguzi mkuu wa 2015. Kura na vigezo vimeanishwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 7: Sifa na Vigezo vya Raisi atakayefaa kuchaguli kwa mwaka 2015

Na.	Sifa na Vigezo vya Raisi	Kura zilizopigwa	Asilimia(%)
1	Umri na mzoefu kazini	254	7.7
2	Muadilifu	1106	33.53
3	Mtendaji kwa vitendo	1619	49
4	Elimu	200	6
5	Mapenzi na chama kwanza na itikadi	78	2.4
6	Sifa nyinginezo	31	0.9
Jumla ya Kura zilizopigwa		**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Kutokana na kura zilizopigwa kuhusu sifa na vigezo vya Raisi atakayefaa, sifa na kigezo cha utandaji kwa vitendo kimechukua nafasi kubwa na kupata kura 1619 (49%) ya kura zote zilizopigwa. Hii inadhirisha kuwa, raisi anayetarajiwa lazime awe na sifa au historia ya utendaji kwa vitendo vinavyodhirika. Hata hivyo, jumla ya kura **1106 (33.53%)** zilionesha kuwa wananchi wanahitaji Raisi muadilifu ambaye ataweza kuaminika. Ikilinganishwa na takwimu katika jedwali nambari 6 hapo juu, ni dhahiri kuwa wananchi wamechoka na rushwa na ufisadi kama ilivyodhirika kwa kuwa na kura **1097(33.26%)**. Hii inamaanisha kuwa, Raisi atakayefaa ni yule mwenye dhamira ya wazi ya kutekeleza majukumu yake kwa vitendo na siyo ushabizi wa chama. Kwa mfano, kwa upande wa sifa na kigezo cha ***"mapenzi ya chama na itikadi"***, kura zilizopigwa ni 78 (2.4%), hii inamaanisha kuwa, wananchi wanaangalia utendaji zaidi na siyo sifa ya kuwa na mapenzi ya chama, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeloe ya nchi. Elimu ni msingi na ufunguo wa maendeleo. Ijapokuwa kigezo hiki kimechukua nafasi ndogo; kura 200 (6%) haina maana kuwa kuwa Raisi awe na elimu ndogo isiyomuwezesha kuwa na dira na maono makubwa ya nchi. Kwa kuwa swala la elimu limeonekana kuwa ni kipaumbele kikuu katika utafiti huu, ingelifaa kuwa na Raisi mwenye elimu nzuri inayomuwezesha kujiamini katika kufanya maamuzi yake.

7.2.3. Sifa na Vigezo vya kiongozi anayefaa kuwa Mbunge 2015

Katika utafiti huu, swali nambari 7 lililenga kujua sifa na vigezo vya kiongozi anayefaa kuwa Mbunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania. Swali hili lilikuwa na vidokezo 7 ambavyo washiriki wa utafiti walichagua kadri ya maoni yao. Vidokezo hivyo ni pamoja na: uzoefu

kazini, uadilifu, mapenzi ya chama na itikadi, utendaji kwa vitendo, elimu, umri na umaarufu. Kutokana na kura zilizopigiwa, matokeo ya utafiti yamebaini kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali Nambari 8: Sifa na Vigezo vya Mbunge atakayefaa,2015

Na.	Sifa na Vigezo vya Mbunge	Kura zilizopigwa	Asilimia(%)
1	Uzoefu kazini	211	6.4
2	Muadilifu	1175	35.6
3	Mtendaji kwa vitendo	1595	48.4
4	Elimu	163	4.9
5	Mapenzi na chama kwanza na itikadi	102	3.1
6	Umri	24	0.73
7	Umaarufu	28	0.85
Jumla ya Kura zilizopigwa		**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Kutokana na matokeo hayo, sifa na kigezo kikuu cha **Mbunge atayefaa** kuongoza jimbo ni yule aliye na sifa ya utendaji kwa vitendo dhahiri; ambapo kwa sifa hii jumla ya kura 1595 (48.4%) zilipigwa. Hii inamaanisha kuwa kuwa, wananchi (wapiga kura) wanatazama sifa kuu ya uchapa kazi na historia ya kutimiza ahadi kwa wapiga kura. Sambamba na sifa hiyo, swala la uadilifu limechukua nafasi ya pili ambapo jumla ya kura 1175 (35.6%) zilipigwa. Kutokana na matokeo haya, uadilifu na utendaji kwa vitendo ndiyo vigezo na sifa kuu za kumchagua Mbunge. Ni dhahiri kuwa, sifa hizi mbili zinashabihiana katika uhalisia wa maisha. Ikilinganishwa na sifa na vigezo vingine kama vile umaarufu (0.845) na ushabiki wa kichama (3.1%); sifa hizi mbili zimechukua

nafasi ya chini sana katika utafiti huu. Hii inamaanisha kuwa, matarajio ya wapiga kura siyo umaarufu wa mtu binafsi wala ushabiki wa chama. Matajio ya wananchi ni kupata kiongozi mwaminifu, muadilifu wa mali za umma, mtetezi wa wananchi, na mwenye historia ya utendaji kwa vitendo.

Swala la umri halikuwa ni kigezo kikubwa kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu ambapo kura 24 zilipigwa sawa na asilimia 0.73. Swala la elimu ya kiongozi ni muhimu sana kwa ajili ya uwezo wa utendaji. Hata hivyo, katika utafiti huu, elimu ya kiongozi ilipata kura 163 (4.9%). Kwa upande mwingine uzoefu wa kiongozi ulichukua nafasi maalumu. Kutokana na matokeo ya utafiti huu jumla ya kura 211 zilipigwa kuonesha umuhimu wa uzoefu wa Mbunge. Kwa ujumla, kipengele cha uzoefu wa kiongozi kipata asilimia 6.4.

7.2.3. Sifa na Vigezo vya kiongozi anayefaa kuwa Diwani

Nafasi ya Diwani katika ngazi ya uongozi wa kata ni nguzo muhimu sana katika kutekeleza ilani ya chama chake. Diwani analo jukumu kubwa na kuhamasisha maendeleo ya kata husiki na kufuatilia mwenendo wa watendaji wa serikali katika kata katika maeneo ya afya, elimu, ardhi, na kulinda na kutetea haki za wananchi. Swali nambari 6 katika dodoso la utafiti lililenga kujua sifa na vigezo vya kumchagua Diwani katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka 2015 nchini Tanzania. Jumla ya vidokezo 7 vilipigiwa kura na wananchi walioshiriki katika utafiti huu. Vidokezo hivyo ni pamoja na: uzoefu kazini, uadilifu, mapenzi ya chama na itikadi, utendaji kwa vitendo, elimu, umri na umaarufu. Kwa mujibu wa kura zilizopigwa, matokeo ya utafiti yanaonesha kama ilivyo kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Nambari 9: Sifa na Vigezo vya Diwani atakayefaa,2015

Na.	Sifa na Vigezo vya kuchagua Diwani	Kura zilizopigwa	Asilimia(%)
1	Uzoefu kazini	245	7.4
2	Muadilifu	1224	37.1
3	Mtendaji kwa vitendo	1473	44.7
4	Elimu	198	6
5	Mapenzi na chama kwanza na itikadi	105	3.2
6	Umri	29	0.87
7	Umaarufu	24	0.73
Jumla ya Kura zilizopigwa		**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Kutokana na matokeo ya utafiti, kuna uwiano mkubwa kati ya matokeo uadilifu na utendaji kwa vitendo. Kwa mujibu wa utafiti huu, jumla ya kura 1473 (44.7%) zilipigwa kwa ajili ya sifa ya kiongozi mchapa kazi na vitendo. Upande mwingine, jumla ya kura 1224 (37.1%) zilipigwa kwa ajili ya sifa ya uadilifu. Sifa hizi pia zimechukua nafasi kubwa sana upande wa Raisi na Mbunge. Hii inamaanisha kuwa wananchi tayari wanajua vigezo watakavyo vitumia kuchagua viongozi katika uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakaofanyika mwaka 2015. Ni dhahiri kuwa wapiga kura majimboni wamechoshwa na porojo, rushwa na ahadi hewa zisizotekelezeka. Katika utafiti huu, uzoefu kazini umeonesha kuchukua nafasi ya tatu kwa ngazi ya Diwani; kwa kuwa na kura 245(7.4%) . Pengine hii inamaanisha kuwa na kiongozi anayejua matatizo ya wananchi mahali pake na kwenye kata husika. Ushabiki wa ki-itikadi za chama, umaarufu binafsi na umri havikuwa vigezo vikuu katika utafiti huu. Swala la elimu ya kiongozi limechukua nafasi ya nne kwa nafasi ya Diwani ambapo jumla ya kura 198 (6%) zilipigwa. Elimu ni ufunguo wa maisha; hivyo, Diwani apaswa kuwa na elimu ya kutosha kupambanua changamoto za kata yake.

8.0. MAONI JUU YA KIONGOZI ANAYEFAA KUWA RAISI , 2015

Muundo wa utafiti huu ulizingatia hali halisi ya kisiasa nchini Tanzania hasa kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2015. Pamoja na kwamba Tume ya Uchaguzi (NEC) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijatangaza rasmi muda wa kuanza kampeni za uchaguzi na wanasias kujinadi kwa wapiga kura majimboni na maeneo mengine; hata hivyo, tayari kuna harakati za awali (mbio za chini chini) za baadhi ya viongozi wa kisiasa na walio

katika utumishi wa umma (walioko madarakani na wastaafu) wameanza kuonesha nia zao za kuwania nafasi ya Uraisi mara tu baada ya muhula wa Raisi wa awamu ya nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete atakapostaafu nafasi hiyo.

Pamoja na wanasiasa hao kuanza mbio za chini chini, ipo minong'ono ya wananchi juu ya nani atakaye mrithi Raisi Jakaya Kikwete. Ili kujua maoni ya wananchi (wapiga kura) juu ya nani anafaa kuwa mrithi wa Raisi Kikwete kwa kufuatana na sifa na vigezo vilivyopendekezwa katika utafiti huu, taasisi ya "***Positive Thinkers Tanzania"***; ilitafuta maoni kwa wananchi juu ya nani ataingia katika kupigiwa kura katika utafiti huu. Baada ya kujadiliana na wadau mbali mbali kuzingatia kigezo cha wanasiasa walioonesha nia ya wazi kugombea uraisi, wanaozungumziwa wanaweza kufaa na walioanza kujinadi kwa mbio za chini chini. ***Jumla ya majina 15 ya wanasiasa mashuhuri nchini*** yalipendekezwa kuingia katika utafiti huu ili yapigiwe kura kujua ni mwanasiasa yupi ambaye wananchi wanaona atafaa kuwa Raisi mtarajiwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Majina 15 hayo yalipendekezwa kwa muono na mtazamo wa wanasiasa ambao wameonyesha dhamira ya wazi wazi kutaka kuchukua fomu za kugombea uraisi na wengine kuombwa na wananchi kwa mitazamo ya kisiasa.

Kwa kuzingatia lengo kuu la utafiti ambalo lilikuwa ni "***Kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania".*** Pamoja na malengo mengine mahususi, jukumu mojawapo la utafiti lilikuwa ni *"Kutathimini kiongozi mwenye mvuto anayefaa kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uchaguzi utakaofanyika mwaka 2015."* Matokeo ya utafiti juu ya wanasiasa anayefaa kuwa Raisi ni ilivyoneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 10: Mwanasiasa Anayefaa kuwa Raisi,2015

Na.	Jina la Kiongozi	Wadhifa/ Sifa ya Kiongozi	Jumla ya Kura	Asilimia (%)
1	Mh. Edward N. Lowassa	Waziri Mkuu Mstaafu na Mbunge wa Monduli,CCM	752	22.8
2	Mh. Wilbrod Slaa	Katibu Mkuu Taifa-CHADEMA	644	19.5
3	Mh. Mwigulu Nchemba	Naibu Waziri wa Fedha na Naibu Katibu Mkuu Taifa-CCM	350	10.6
4	Mh. Ibrahimu Lipumba	Mwenyekiti Taifa -CUF	294	8.9
5	Mh. Zitto Kabwe	Mbunge, CHADEMA	224	6.7
6	Mh. John P. Magufuli	Waziri, Wizara ya Ujenzi,CCM	227	6.8
7	Mh. Bernard Membe	Waziri wa Mambo ya Nje, CCM	197	5.9
8	Mh. Mizengo Pinda	Waziri Mkuu, CCM	107	3.2
9	Mh. January Makamba	Naibu Waziri, Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Mbunge Bumbuli,CCM.	54	1.6
10	Mh. Mark Mwandosya	Waziri asiye na Wizara Maalumu	40	1.2
11	Mh. James Mbatia	Mwenyeki- Taifa, NCCR-Mageuzi	34	1.0
12	Mh. Hussein Mwinyi	Waziri wa Ulinzi na JKT	31	0.9
13	Mh. Steven Wassira	Waziri wa Kilimo	16	0.4
14	Mh. Fredrick Sumaye	Waziri Mkuu Mstaafu, CCM	10	0.3
15	Mh. Samwel Sitta	Waziri wa Uchukuzi	72	2.2
16	**Waliosema Sina Kura**		**79**	2.4
17	**Waliosema Yeyote Atakayechaguliwa**		**167**	5.1
JUMLA YA KURA ZILIZOPIGWA			**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, zipo ishara ambazo wapiga kura wanaziona juu ya nani anafaa kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu ya Tano. Katika dodoso la utafiti, kulikuwa na vidokezo viwili ambavyo vilitoa nafasi kwa wapiga kura ambao hawakuwa na uchaguzi kwa mtu yeyote (waliosema *"**Sina Kura**"***).** Waliosema sina kura walikuwa 79 (2.4%); Kwa upande mwingine, kuna kundi la wapiga kura ambao walisema *" **Yeyote Atakayechaguliwa"*** ni sawa. Jumla ya kura zilizopigwa kwa kidokezo hiki zilikuwa 167 (5.1%). Hii inaashiria kuwa, kuna kundi kubwa la wapiga kura ambao wako njia panda au hawajui nani anaweza kufaa kuwa Raisi endapo moja ya majina yaliyotajwa hapo yataingia katika kinyang'anyiro cha nafasi ya Raisi. Kwa misingi hiyo, inawezekana kuna kundi kubwa la wapiga kura ambalo linahitaji elimu ya uraia

zaidi kabla ya kupiga kura au wamekosa mwelekeo kutokana na hali ya siasa, sifa na vigezo vya wanasiasa wenyewe.

8.1. Nani Anafaa Kuwa Raisi wa Awamu ya Tano?

Kwa mujibu wa utafiti huu, jina lililoongoza kwa kura ni **Mheshimiwa Edward Lowassa** (CCM) ambaye alipata kura 752 (22.8%). Kutokana na sampuli ya wapiga kura wote(3298) kutoka mikoa 13 iliyoshiriki katika utafiti huu, inamaanisha kuwa wapiga kura wengi(bila kujali itikadi za vyama) wanaimani kubwa na Mh. Edward Lowassa kuwa Raisi wa Tanzania katika awamu ya tano. Nafasi ya pili ilichukuliwa na **Mheshimiwa Wilbrod Slaa** (CHADEMA) aliyepata kura 644 (19.5%). Kwa kulinganisha nafasi ya kwanza na ya pili, kuna tofauti ya kura 108 alizopata Mh. Lowassa zaidi ya Mh. Wilbrod Slaa. Nafasi ya tatu ilichukuliwa na **Mheshimiwa Mwigulu Nchemba** (CCM) aliyepata kura 350 (10.6%).

Nafasi ya nne ilichukuliwa na **Mh. Ibrahimu Lipumba** kwa kupata kura 294 (8.9%). Nafasi ya tano ilichukuliwa na **Mh. John P. Magufuli** kwa kura 227 (6.8%), nafasi ya sita ilichukuliwa na **Mh. Zitto Kabwe** kwa kura 224 (6.7%). Nafasi ya saba ilichukuliwa na **Mh. Bernard Membe** ambaye alikuwa na kura 197 (5.9%), nafasi ya nane ilichukuliwa na **Mh. Mizengo Pinda** (Waziri Mkuu katika serikali ya awamu ya nne inayoongozwa na Mheshimiwa Raisi Jakaya Mrisho Kikwete) ambaye alipata kura 107 (3.2%). Kwa upande mwingine, nafasi ya tisa ilishikwa na Mh. Samwel Sitta kwa kura 72 (2.2%). Nafasi ya kumi ilishikwa na **Mh. January Makamba** (Naibu Waziri, Wizara ya Sayansi na Teknolojia) ambaye alipata kura 54 (1.6%) ya kura zote zilizopigwa. Nafasi ya kumi na moja ilishikwa na **Mh. Mark Mwandosya** aliyepata kura 40 (1.2%). Nafasi ya kumi na mbili ilichukuliwa na **Mh. James Mbatia** aliyepata kura 34 (1%). Kwa upande mwingine, nafasi ya kumi na tatu ilishikwa na **Mh. Hussein Mwinyi** aliyepata kura 31 (0.9%). Nafasi ya kumi na nne ilishikwa na **Mh. Steven Wassira** ambaye alipata kura 16 (0.4%). Kwa upande mwingine, nafasi ya kumi na tano katika mtiririko wa kura ilishikwa na **Mh. Fredrick Sumaye** (Waziri Mkuu Mstaafu, serikali ya awamu ya tatu) ambaye alipata 10 (0.3%) kati ya kura 3298.

Hata hivyo, katika ujumla wake, mwanasiasa aliyeongoza kwa kura nyingi ni **Mh. Edward Lowassa**; ambaye anaonekana kuwa na kura nyingi (752) sawa na asilimia 22.8 ya kura zote. Kwa maana nyingine, Mh. Lowassa(CCM), aliongoza kwa kura nyingi akifuatiwa na **Mh. Wibrod Slaa**

(CHADEMA) aliyepata kura 644 sawa na asilimia 19.5 ya kura zote zilizopigwa. Kwa kulinganishwa na sifa na vigezo vilivyotajwa katika jedwali Na. 7 hapo vya kiongozi anayefaa kuwa Raisi kuelekea uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; swala la ***"Utendaji kwa vitendo"*** lilichukua nafasi kubwa likifuatiwa na ***"Uadilifu wa kiongozi".*** Hivyo ndivyo vigezo vikuu vilivyopendekezwa na wapiga kura kutoka mikoa 13 iliyoshiriki katika utafiti huu.

8.2. Idadi ya Kura Kwa Wanasiasa Kulingana na Itikadi ya Chama

Utafiti huu umebaini kuwa, kura zilizopigwa hazikuwa na mlengo wa ki-itikadi ya vyama kwa wapiga kura zaidi ya kuzingatia vigezo na sifa za mwanasiasa mwenyewe aliyependekezwa jina katika dodoso la utafiti huu. Hivyo, wapiga kura walitumia uhuru wao wa kuamua bila kujali maslahi ya vyama vyao kama iliyooneshwa kwenye jedwali Na. 11, hapo chini.

Jedwali Na. 11: Kura Kulingana na Itikadi ya Vyama kwa Wanasiasa

Na.	JINA LA MWANASIASA	IDADI YA KURA ZILIZOPIGWA NA WASHIRIKI KUTOKA VYAMA VYA SIASA KWA WANASIASA						
		CCM	CHADEMA	CUF	NCCR-M	SINA CHAMA	VYAMA VINGINE	Jumla
1	Mh. Edward Lowassa	493	143	13	7	90	6	752
2	Mh. Wibrod Slaa	17	555	13	5	54	0	644
3	Mh. Mwigulu Nchemba	126	70	44	34	39	37	350
4	Mh. Ibrahim Lipumba	17	20	224	6	24	3	294
5	Mh. John Magufuli	97	56	16	2	55	1	227
6	Mh. Zitto Kabwe	17	160	10	2	31	4	224
7	Mh. Bernard Membe	122	22	22	2	27	2	197
8	Mh. Mizengo Pinda	71	28	0	1	5	2	107
9	Mh. January Makamba	31	8	3	0	12	0	54
10	Mh. Mark Mwandosya	21	10	1	1	7	0	40
11	Mh. James Mbatia	3	8	2	15	6	0	34
12	Mh. Hussein Mwinyi	16	0	6	1	7	1	31
13	Mh. Steven Wassira	8	2	0	0	6	0	16
14	Mh. Fredrick Sumaye	5	1	0	0	4	0	10
15	Mh. Samwel Sitta	47	6	2	0	14	3	72
16	**Sina Mgombea**	**13**	**11**	**0**	**0**	**54**	**1**	**79**
17	**Kiongozi Yeyote**	**40**	**17**	**4**	**1**	**103**	**2**	**167**
Jumla		**1144**	**1117**	**360**	**77**	**538**	**62**	**3298**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Matokeo ya utafiti huu , jedwali Na. 11 hapo juu, yanaonesha dhahiri kuwa, ijapokuwa wananchi wengi walioshiriki katika utafiti huu walijitambulisha kwa itikadi za vyama vyao, hata hivyo wengi wao walikuwa na uhuru wa kuchagua jina la mwanasiasa bila kujali itikadi ya chama kama

inavyoonekana hapo juu. ***Ndiyo maana, dhana ya wanasiasa walio wengi kudhani kuwa wanaweza kupigiwa kura na wanachama wa vyama vyao kulingana na itikadi zao sasa haina matumaini tena.*** Kwa mfano: jumla ya washiriki 143 kutoka CHADEMA walimpigia kura Mh. Edward Lowassa. Pia kura 44 kutoka CUF zilipigwa kwa ajili ya Mh. Mwigulu Nchemba, 17 kutoka CCM kwenda kwa Mh. Wilbrod Slaa, kura 90 kutoka kwa washiriki wa utafiti wasio na itikadi yoyote walimpigia Mh. Edward Lowassa. Pia, kura 54 kutoka kwa washiriki wasiokuwa na chama wala itikadi yoyote walimpigia Mh. Wilbrod Slaa. Kwa upande mwingine, kura 28 kutoka kwa wanachama wa CHADEMA walimpigia Mh. Mizengo Pinda (CCM), na kura 34 za wanachama wa NCCR-Mageuzi walimpigia Mh. Mwigulu Nchemba (CCM). Mtazamo huu unaonyesha dhahiri kuwa wanasiasa wanaweza kuona picha nyingine kuwa lengo si kuwa na mapenzi na itikadi ya vyama bali ni uwezo wa kutenda na uadilifu ndivyo vinavyoonekana vya msingi katika wananchi wapiga kura. Pamoja na kura zilizopigwa, hata hivyo, utafiti huu umebaini kuwa wapo wananchi wengi wasio na itikadi yoyote lakini wako makini kuchagua kiongozi anayefaa. Kwa mfano, jumla ya **washiriki 538** (kama ilivyooneshwa katika jedwali Na. 11 hapo juu) hawakuwa na mlengo wowote wa ki-chama.

9.0. CHAMA CHA SIASA CHENYE MVUTO NA KUKUBALIKA KWA WANANCHI

Pamoja na kuangalia mwanasiasa anayefaa kuwa Raisi kuelekea uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; utafiti huu pia ulilenga kujua maoni ya wananchi kuhusu chama chenye mvuto kulingana na sera zake kitaifa. Katika dodoso la utafiti, swali Na. 2, lilihoji kuhusu chama chenye mvuto (chama cha siasa kinachokubalika kwa wananchi). Kutokana na kura zilizopigwa na washiriki wa utafiti, matokeo ya utafiti yameoneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 12: Chama cha siasa chenye Mvuto nchini

Na	Chama cha Siasa	Kura zilizopigwa	Asilimia (%)
1	Chama Cha Demokrasia na Maendeleo, CHADEMA	1471	44.6
2	Chama Cha Mapinduzi, CCM	1136	34.4
3	Civic United Front, CUF	348	10.6
4	NCCR-Mageuzi	61	1.8
5	Sina Chama	251	7.6
6	Vyama Vingine Vya Siasa	31	0.9
Jumla ya Kura Zilizopigwa		3298	100

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Kulingana na kura zilizopigwa, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa chama cha siasa nchini kilichochukua nafasi ya kwanza kuwa na mvuto mkubwa kwa wananchi ni **Chama Cha Demokrasia na Maendeleo,** CHADEMA; ambacho kilipata kura 1471 (44.6%). Kikifuatiwa na **Chama Cha Mapinduzi (CCM)** kilichochukua nafasi ya pili kwa kura 1136 (34.4%). Nafasi ya tatu kwa mvuto ilichukuliwa na **Civic United Front (CUF)** kwa kura 348(10.6%); na nafasi ya nne ilichukuliwa na **NCCR-Mageuzi** kwa kura 61 (1.8%). Hata hivyo, utafiti ulibaini kuwa wapo wananchi wengi wasio na uchabiki,ufuasi wala mvuto wa chama chochote cha siasa. Kundi hili la wananchi lilijibu ***"Sina Chama",*** ambapo jumla ya kura 251 (7.6%) zilipigwa na washiriki wa utafiti wasio na chama cha siasa.

Kwa upande mmoja, matokeo haya yanaweza kuleta tafsiri kuwa, huenda wananchi hawa hawana elimu ya uraia na hawajahamasika na na maswala ya ushiriki katika siasa. Kwa upande wa pili inaweza kuonesha kuwa wananchi wamechoka na siasa zisizowafikisha katika hatima za maendeleo ya nchi yao. Pengine, inahitajika mfumo mpya wa fikra kwa wananchi. Kwa upande mwingine, jumla ya kura 31 (0.9%) zilionesha kuwa wananchi wana mvuto na vyama vingine walipopiga kura ya ***"Vyama Vingine".*** Kimsingi, vyama vikuu vya siasa nchini vilivyopewa kipaumbele katika kupima mvuto wa chama ni pamoja na CCM, CHADEMA, CUF na NCCR-Mageuzi.

9.1. Mtawanyiko wa Kura zilivyopigwa Kwa Chama Chenye Mvuto

Jedwali Na. 13: Mtawanyiko wa kura kwa Chama Chenye Mvuto

Chama Cha Mshiriki	**Kura Kwa Chama Chenye Mvuto**						
	CCM	CHADEMA	CUF	NCCR-M	SINA CHAMA	VYAMA VINGINE	**Jumla**
CCM	939	171	25	0	6	3	**1144**
CHADEMA	66	1011	23	9	8	0	**1117**
CUF	20	59	276	1	3	1	**360**
NCCR-Mageuzi	11	24	2	39	0	1	**77**
SINA CHAMA	97	181	21	6	229	4	**538**
VYAMA VINGINE	3	25	1	6	5	22	**62**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti kama ilivyooneshwa kwenye jedwali Na. 13 hapo juu, inaonesha kuwa siyo washiriki wote wa chama fulani cha siasa walipendelea vyama vyao. Kwa mfano: washiriki 171 wa CHADEMA walisema kuwa CCM ndiyo chama chenye mvuto zaidi nchini, wakati huo washiriki 66 wa CCM walipigia kura CHADEMA. Kwa upande mwingine, kura 25 kutoka CUF zilipigwa kwa ajili CCM kuwa ndicho chama chenye mvuto na kura 59 kutoka CHADEMA zilipigwa kwa CUF. Matokeo haya yanabaini kuwa siyo itikadi ya chama ndiyo inayoongoza mpiga kura kufanya maamuzi; bali ni jinsi aonavyo chama chenye mvuto bila kujali ushabiki. Hata hivyo, kura 9 kutoka NCCR-Mageuzi zilipigwa kwa ajili ya CHADEMA. Wakati huo huo, kura 229 zilisema ***" Sina Chama Chenye Mvuto";*** hii inaleta picha kuwa, kuna kundi kubwa la wananchi ambalo halina ushabiki wa ki-itikadi badala yake wapiga kura hao wanaangalia msimamo wao juu ya mgombea.

Hali hii inaashiria kuwa, kampeni za uchaguzi zisiangalie itikadi zaidi bali zizingatie makundi mengine hata ambayo hayana vyama vya siasa lakini yanauelewa wa kufanya maamuzi juu ya hatima ya nchi. Kwa upande mwinge, vyam vingine vya siasa vipipata jumla ya kura 62 tu. Pengine ni kwa sababu ya uchanga au uchache wa wanachama katika mikoa iliyoshiriki utafiti huu. ***Matokeo ya kushangaza kutoka kwa washirki wote bila kujali itikadi za vyama vyao ni kuwa, jumla ya kura 538, sawa na asilimia 16.3 ya kura zote zilionesha hakuna chama chenye mvuto kabisa nchini.***Hii inaweza kuleta picha kuwa, japo kuna vyama vingi nchini, wananchi wamekosa mwelekeo na vyama vya siasa; pengine vyama vyao havijakidhi mahitaji yao na kuleta hamasa ya maendeleo na hatima ya nchi yao. *Katika mada zilizopita, maswala ya uaminifu, uadilifu, utendaji kwa vitendo na uwajibikaji wa viongozi yalipewa nafasi kubwa kuwa vigezo vya msingi kumchagua kiongozi kwa ngazi za Diwani, Mbunge na Raisi*. Pengine hayo ndiyo mambo ambayo wananchi wangependa

kuyaona kutoka kwa viongozi wa siasa; na kwamba wanayatazama kwa jicho la upeo wa juu na mwelekeo mkubwa wa siasa nchini Tanzania.

10.0. SIFA ZA WASHIRIKI WA UTAFITI

Ili kutambua mtazamo na sifa za wapiga kura, itikadi za chama na umri, timu ya utafiti iliwahoji wananchi walioshirki katika utafiti juu ya kiwango cha elimu, umri na itakadi.Lengo lilikuwa ni kuangalia mwamko wao kisiasa na jinsi wanavyoshiriki katika kufanya maamuzi. Sehemu zifuatazo zinaainisha sifa za washiriki kwa kufuata umri, elimu na itakadi za chama.

10.1. Elimu ya Washirki

Utafiti ulishirikisha ngazi zote na tabaka zote kwa walio na elimu na wasio na elimu kabisa. Utafiti uliweka vigezo vya elimu kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 14: Kiwango Cha Elimu ya Washiriki

Na	Kiwango cha Elimu	Jumla ya Washiriki	Asilimia(%)
1	Sina Elimu	175	5.3
2	Elimu ya Msingi	980	29.7
3	Elimu ya Sekondari	1112	33.7
4	Elimu ya Cheti/Stashahada	609	18.5
5	Elimu ya Chuo Kikuu	422	12.8
Jumla ya washiriki		3298	100

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, kundi kubwa la walioshiriki katika utafiti huu ni wenye elimu ya sekondari ambao jumla walikuwa 1112 (33.7%), wakifuatiwa na wenye elimu ya msingi ambao

walikuwa 980 (29.7%). Kwa upande mwingine, nafasi ya tatu ilikuwa ni kundi la wenye elimu ya cheti na stashahada ambao ni 609 (18.5%). Hii inamaanisha kuwa kuna mwamko mkubwa sana wa kisiasa kwa wananchi (wapiga kura) walio katika makundi ya elimu ya sekondari, cheti na stashahada. Kwa upande wa elimu ya chuo kikuu walikuwa 422 (12.8%). Hili ni kundi muhimu sana kisiasa kutokana na hali halisi kuwa wana elimu kubwa na ufahamu wa juu.

10.2. Umri wa washiriki

Katika utafiti huu, umri uliozingatiwa ni kati ya miaka 18 hadi 60, na zaidi. Kipengele hiki kilizingatia kanuni ya umri ulioruhusiwa kisheria kupiga kura. Kwa hiyo, umri wa washirki wa utafiti huu uliwekwa katika makundi makuu matano kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 15: Umri wa Washiriki

Na	Umri Katika Miaka	Jumla ya Washiriki	Asilimia(%)
1	Miaka 18 hadi 24	688	20.9
2	Miaka 25 hadi 34	973	29.5
3	Miaka 35 hadi 44	824	24.9
4	Miaka 45 hadi 60	564	17.1
5	Miaka zaidi ya 61	249	7.6
Jumla ya washiriki		**3298**	**100**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015



Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, kundi kubwa kwa kigezo cha umri lililoshiriki katika utafiti ni lile lililoko kati ya miaka 25 hadi 34 ambalo lilikuwa na idadi ya washirki 973 (29.5%). Kundi la pili kwa idadi na umri ni wale wenye miaka kati ya 35 hadi 44 waliokuwa 824 (24.9%). Matokeo haya yanaambatana na hali halisi ya kiwango cha elimu ambapo katika jedwali Na 14, limeonesha kuwa wapiga kura wengi ni wale walio na elimu ya sekondari wakifuatiwa na wenye elimu ya shule ya msingi. Kwa upande mwingine, asilimia 20.9 ni wale wenye umri kati ya miaka 18 hadi 24. Idadi hii ni kundi kubwa sana la vijana. Miaka kati ya 45 hadi 60 walikuwa asilimia 17.1. Hili ni kundi la watu wazima; na asilimia 7.6 tu ilikuwa ni kundi la wazee wenye umri zaidi ya miaka 61.

Kwa maana nyingine, matokeo ya utafiti yanaashiria kuwa, '***watu wenye umri wa miaka 18 hadi 45 ni kundi kubwa sana lenye maamuzi mazito ya hatima ya nchi na uongozi kwa ujumla'.***

11.0. IDADI YA KURA ALIZOPIGIWA MWANASIASA MASHUHURI KWA KILA MKOA

Kufuatana na matokeo ya utafiti, kila mkoa ulionesha uwingi wa kura za kila mwanasiasa. Hii haimaanishi kuwa, mkoa fulani unaupendeleo na mwanasiasa fulani, bali ni jinsi wananchi walivyopiga kura zao kulingana na vigezo vilivyopo na kadri wapiga kura walivyoona anafaa. Hivyo, jedwali hapo chini linaonesha mtawanyiko wa idadi ya kura kwa kila mkoa kwa kila mwanasiasa mashuhuri aliyeonesha nia ama wananchi wanamnong'ona kuwa anafaa kuwa kiongozi wa nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jedwali Na. 16: Idadi ya Kura Ki-Mkoa kwa Kila Mwanasiasa

Na.	JINA LA MWANASIASA	IDADI YA KURA KI-MKOA KWA MWANASIASA												
		DSM	AR	MW	MB	MT	TG	L	D	PW	IR	KL	SH	MR
1	Mh. Edward Lowassa	166	169	63	62	37	39	11	61	41	40	50	13	-
2	Mh. Wibrod Slaa	151	61	110	76	16	24	9	43	21	56	49	27	1
3	Mh. Mwigulu Nchemba	83	20	18	5	17	38	14	30	55	16	19	34	1
4	Mh. Ibrahim Lipumba	79	5	4	-	50	35	72	10	14	15	5	4	
5	Mh. John Magufuli	66	14	42	17	5	17	3	9	12	9	26	7	
6	Mh. Zitto Kabwe	79	10	12	6	36	12	14	13	3	9	14	16	
7	Mh. Bernard Membe	61	8	7	1	16	11	68	4	11	5	4	1	
8	Mh. Mizengo Pinda	21	4	15	17	1	5	5	4	11	11	7	6	
9	Mh. January Makamba	31	6	-	4	1	4	-	1	3	2	2	-	
10	Mh. Mark Mwandosya	8	2	-	16	3	1	1	3	1	3	1	1	
11	Mh. James Mbatia	12	5	2	2	4	2	1	-	-	3	3	-	
12	Mh. Hussein Mwinyi	13	13	1	2	-	4	-	3	2	3	1	2	
13	Mh. Steven Wassira	6	1	2	1	-	-	-	-	-	3	2	-	
14	Mh. Fredrick Sumaye	5	2	-	-	-	-	-	1	-	-	2	-	
15	Mh. Samwel Sitta	28	3	4	5	3	3	1	7	2	5	3	8	
16	Sina Mgombea	16	9	6	**5**	**12**	**6**	**-**	**7**	**6**	**8**	**1**	**-**	
17	Kiongozi Yeyote	60	6	16	**18**	**13**	**7**		**6**	**17**	**7**	**6**	**5**	
Jumla Ya Kura		**885**	**325**	**302**	**238**	**214**	**208**	**207**	**202**	**199**	**195**	**195**	**126**	**2**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Kielelezo cha Majina:

DSM= Dar es Salaam, AR= Arusha, MW= Mwanza, MT= Mtwara, MB= Mbeya, TG= Tanga, L= Lindi, D= Dodoma, PW= Pwani, IR= Iringa, KL= Kilimanjaro, SH= Shinyanga, na MR= Morogoro.

Kutokana na matokeo ya utafiti, kila mwanasiasa amonekana ana umaarufu katika mikoa fulani hapa Tanzania bara. Kwa mfano: **Mh. Edward Lowassa** alipata kura nyingi katika mikoa ya Dar es Salaam(166), Arusha (169), Mwanza (63), Mbeya (62), Iringa (40) and Kilimanajro (50). Kwa upande mwingine, **Mh. Wilbrod Slaa** alikuwa na kura nyingi katika mikoa ya Dar es Salaam (151), Mwanza (110), Mbeya (76), Iringa (56) na Kilimanjaro (49). Wakati huo huo kura zinaonesha kuwa, katika mikoa iliyoshiriki kupiga kura katika utafiti huu **Mh. Mwigulu Nchemba** alikuwa na kura nyingi katika mikoa ya Dar es Salaam (83), Pwani (55), Tanga (38) na Shinyanga (34). Hata hivyo, kwa upande wa CUF, **Mh. Ibrahimu Lipumba** alikuwa na kura nyingi mikoa ya Mtwara (50), Dar es Salaam (79), Lindi (72), na Tanga (35). **Mh. John Magufuli** alikuwa na kura nyingi mikoa ya Mwanza (42), Dar es Salaam (66) na Kilimanjaro (26). Kwa upande wa **Mh. Bernard Membe**, yeye alipata kura nyingi mikoa miwili ambayo ni Dar es Salaam (61) na Lindi (68).

Kwa upande wa **Mh. Mizengo Pinda**, kwa Dar es Salaam alipata jumla ya kura 21 na mkoa wa Mbeya alipta kura 17. Wakati huo, **Mh. January Makamba** alipata kura 31 mkoani Dar es Salaam na kura 6 mkoa wa Arusha. Kwa ujumla, Mh. Edward Lowassa ameongoza kwa kupata kura nyingi katika mikoa mingi iliyoshiriki; akifuatiwa na Mh. Wilbrod Slaa.

12. KIGEZO CHA ELIMU NA JINSI WALIVYOPIGA KURA

Utafiti ulibaini kuwa upo uhusiano kati ya elimu ya wapiga kura na jinsi wanavyoweza kufanya maamuzi ya kuchagua kiongozi. Jedwali lifuatalo linaonesha wanasiasa waliochukua nafasi tatu za mwanzo katika wingi wa kura.

Jedwali Na. 17: Kigezo cha Elimu walivyopiga kura kwa wanasiasa watatu wa kwanza

Na	Jina la Mwanasiasa	Kiwango Cha Elimu ya Washiriki/ Wapiga Kura					Jumla
		Darasa la I-VII	Kidato Cha I-VI	Cheti/ Stashahada	Chuo Kikuu	Sina Elimu	
1	Mh. Edward Lowassa	262	242	104	108	36	**752**
2	Mh. Wilbrod Slaa	193	252	111	70	18	**644**
3	Mh. Mwigulu Nchemba	26	73	142	93	16	**350**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Kutokana na matokeo ya utafiti uliofanyika katika mikoa 13 Tanzania bara, inaonesha kuwa kwa mujibu wa kiwango cha elimu kuna makundi makuu mawili ya wananchi ambao ndiyo wapiga kura waliowengi. '***Makundi hayo ni wale wenye elimu ya shule ya msingi na wale walio na elimu ya kidato cha lwanza hadi cha sita'.*** Haya ni makundi maalumu ya wapiga kura. Hata hivyo, inaonesha kuwa, makundi haya mawili ndimo walimo vijana walio kati ya umri wa miaka 18 hadi 35 (kwa mujibu ya matokeo ya utafiti huu). ***Swali la msingi hapa linaweza kuwa: Je, wanasiasa wanatambua umuhimu wa makundi haya?***

Kwa mujibu ya matokeo ya utafiti, **Mh. Edward Lowassa** alipata kura nyingi za wananchi wenye elimu ya shule ya msingi (262) na wenye elimu ya sekondari(242). Kwa upande mwingine, **Mh. Wilbrod Slaa** alipata kura nyingi za wananchi wenye elimu ya shule ya msingi (193) na wenye elimu ya sekondari (252). Nafasi ya tatu ilikuwa ya **Mh. Mwigulu Nchemba** ambaye alipata kura nyingi kutoka kwa wapiga kura wenye kiwango cha elimu ya cheti/stashahada (142) wakifuatiwa na wenye elimu ya chuo kikuu (93).

13. KIGEZO CHA UMRI NA JINSI WALIVYOPIGA KURA

Dodoso la utafiti liligawanya umri wa washirki katika makundi makuu matano. Wale wenye wa miaka kati ya 18- 24, 25-34, 35- 44, 45- 60 na wenye umri zaidi ya 60. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha umri wa washirki walivyopiga kura kwa wanasiasa watatu waliopata idadi kubwa ya kura.

Jedwali Na. 18: Kigezo cha Elimu walivyopiga na kura kwa wanasiasa watatu wa kwanza

Na	Jina la Mwanasiasa	Umri wa Washiriki/ Wapiga Kura katika miaka					Jumla
		18- 24	25- 34	35- 44	45- 60	Zaidi ya 60	
1	Mh. Edward Lowassa	160	221	160	148	63	**752**
2	Mh. Wilbrod Slaa	149	224	171	80	20	**644**
3	Mh. Mwigulu Nchemba	35	91	144	51	29	**350**

Chanzo; Utafiti PTT, Februari-Machi 2015

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, **Mh. Edward Lowassa** alipigiwa kura nyingi na wananchi walio kati ya umri wa miaka 25 hadi 34. Kwa mfano, walio na umri kati ya 18- 24 walikuwa 160; na walio na umri kati ya miaka 25 hadi 34 walikuwa 221. Kwa upande mwingine, **Mh. Wilbrod Slaa** alipata kura nyingi za walio na umri kati ya miaka 25 hadi 34 (224) na walio na umri wa miaka 18 hadi 24 walikuwa 149. Wakati huo, **Mh. Mwigulu Nchemba** ameonesha kuungwa mkono na watu wazima zaidi walio na umri kati ya miaka 35 hadi 44 (144) wakifuatiwa na kiasi kidogo cha vijana wenye umri kati ya 25 hadi 34 (91).

Maswali ya msingi hapa ni kwamba***: Je, usemi wa zamani kuwa, "Vijana ni taifa la kesho" bado una nguvu? Je, wanasiasa wanatambua kuwa kundi la vijana ndiyo rasilimali na nguvu kazi ya taifa la Tanzania? Je, vijana wako wapi katika njia kuu za kumiliki uchumi?***

14. HITIMISHO

Utafiti huu hauna mlengo wa ki-itikadi ya chama cha siasa chochote wala hauna madhumuni ya kufanya kampeni kwa mwanasiasa yeyote yule nchini. Utafiti huu umefanywa na shirika lisilo la kiserikali linalojukana kama, "Positive Thinkers Tanzania" (PTT). Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni **"Kutambua vigezo na matarajio ya wananchi katika kufanya maamuzi ya kuchagua viongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania".** Pamoja na changamoto nyingi zilizoonekana kwa pande zote; watafiti na washiriki, matokeo ya utafiti huu yameleta mwaka katika maswala ya maamuzi hasa yanayohusu hatima ya nchi katika kuchagua viongozi watakao faa kuongoza nchi, na wananchi kwa ujumla.

Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa, ijapokuwa wananchi na wanasiasa waliowengi wanadhani kuwa viongozi wa kisiasa watategemea na idadi ya wanachama wenye itikadi zao, yapo makundi ndani ya vyama ambayo yanatambua kuwa itikadi ya chama siyo kigezo bali sifa na vigezo vya kiongozi (mgombea) ndiyo msingi wa kumchagua kiongozi anayefaa kuongoza.

Zipo changamoto nyingi ambazo zimejionesha kutoka kwa wananchi wakati wa kufanya utafiti huu. Kwa mfano:

a) Wananchi wengi hasa vijana kwenye vijiwe (magenge) vya 'Boda Boda' na kahawa walikuwa wakidai wapatiwe chochote ili waweze kutoa ushirikiano. Jambo hili ni changamoto inayotokana na mazoea ya watu kudai chochote hata kwa jambo lenye manufaa ya kueta hatima nzuri kwa nchi yao.
b) Baadhi ya wananchi, hasa mkoani Mtwara walikuwa na hofu ya kushiriki wakidhani utafiti huu umehusisha serikali na hivyo, ni moja ya upelelezi kutambua watu wasiounga mkono chama tawala. Hili lilitokana na vurugu za maswala ya gesi miaka iliyopita.
c) Baadhi ya washiriki waliamini (kwa fikra zao) kuwa mpangilio wa maswali uliegemea chama tawala kwa vile chama tawala (CCM) kimeonekana kuwa cha kwanza kwenye orodha ya maswali kwenye dodoso.
d) Kutokana na umuhimu wa vigezo na vipaumbele vya kumchagua kiongozi, wananchi (washiriki wa utafiti) walio wengi walitaka kuchagua vigezo vyote vilivyopo badala ya

kimoja tu kama ilivyoainishwa kwenye maelezo ya dodoso la utafiti. Hii ilitokana na kero nying za wananchi hazijafanyiwa kazi.

e) Wananchi wengi walikuwa wakisita kutoa maoni/ kushiriki kutokana na kuhisi kuwa utafiti huu unahusiana na kampeni za vyama fulani.

f) Changamoto nyingine ilikuwa lugha ya kiswahili kutofahamika vizuri na baadhi ya jamii, hasa maeneo ya vijijini. Hivyo, ilihitajika kutafuta wakalimani hasa maeneo ya Longido na Monduli.

g) Ushawishi katika makundi. Hili lilijionesha kuwa, endapo kwenye kundi fulani la watu kulikuwa na mtu maarufu ambaye angeliweza kuwashawishi kutoshiriki wenzake; hii ilikuwa ni changamoto. Hivyo, tahadhari ilichukuliwa ili washiriki wasitoe maoni ya ushawishi wa mtu fulani.

h) Ilibainika pia kuwa, katika baadhi ya familia, mume alikuwa na uwezo wa kumshawishi mke kutoa majibu ambayo mme anataka. Kazi kubwa ilifanyika kuwaelewesha washiriki palipokuwa na hali kama hii ili kila mmoja atoe maoni yake binafsi bila kushawishiwa.

i) Baadhi ya wananchi walikataa kushiriki utafiti kutokana na uzoefu wa wanasiasa kutoa ahadi zisizotekelezeka.

Kwa ujumla, malengo ya utafiti huu yametimia. Hata hivyo, utafiti zaidi unahitajika katika maeneo mbali mbali ambayo utafiti huu haukuyafikia. Positive Thinkers Tanzania inapenda kuwashukuru wote waliofanikisha utafiti huu.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na. 1: Dodoso la Utafiti

Kiambatanisho Na.2. Takwimu za Washiriki Wote Kila Mkoa Ulioshiriki Utafiti